

USHIRIKA

Hali ya uzalishaji na mauzo ya kahawa

Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Disemba 2022 Jumla ya tani 812 za kahawa kavu ilipelekwa viwandani kwa ajili ya ukoboaji na baadae kupelekwa kwenye mnada wa kanda ya Songwe. Hadi sasa minada inaendelea kwa upande wa kanda yetu na vyama 12 vya msingi vinatarajia kuuza kupitia minada hiyo.

Aidha Jumla ya vyama ya msingi (AMCOS) 12 vya zao la kahawa ambavyo ni Makoga, Luswisi, Chibila, Bwenda, Kasege, Lubanda, Sange, Ipande, Malangali, Ndatila, Katengele na Gwitonji wamepata pembejeo kwa njia ya mkopo. Jumla ya wanachama 984 kati ya wanachama 1,579 sawa na 62.32 % wamenufaika na mikopo yenyenye thamani ya Tzs. 206,640,000/= ambayo inatarajiwa kulipwa kwa fedha za kahawa msimu wa 2023/24.

Halmashauri ya Wilaya kwa kushirikiana na vyama vya ushirika lleje tunashukuru sana Serikali ya **Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan** kwa kutusogezesa karibu huduma ya Mnada wa zao la kahawa mkoani kwetu Songwe, sisi wana lleje ni jambo la faraja kwani huduma hii ipo maeneo machache ya nchi, hivyo tuunaamini kupitia Mnadaa huu utatuletea mapinduzi makubwa ya kiuchumi na utapunguza adha mbalimbali walizokuwa wakikutana nazo wakulima ikiwepo gharama za usafirishaji.

mafanikio katika sekta ya Ushirika ni kama ifuatavyo:-

1. Wakulima kupata bei ya soko la mnadani moja kwa moja
2. Wakulima kupunguziwa gharama za kusafirisha mazao kwenda moshi mnadani kutokana na mnada kufanyika katika kanda yetu ya Songwe.
3. Upatikanaji wa takwimu sahihi ambazo zimesaidia kuondoa migogoro ya ushuru miongoni mwa Halmashari.
4. Kuwa na sauti ya pamoja kwa lengo la kupata masoko sehemu mbalimbali